



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA NANE LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA ISHIRINI

Kikao cha Kwanza – Tarehe 13 Mei, 2015.

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

- I. **TAARIFA YA SPIKA:**

- II. **HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:**

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais:

Nakala zote za Gazeti Rasmi la Serikali pamoja na vijalizo vyake kuanzia tarehe 1 Aprili, 2015.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora:

Hotuba ya Kuwasilisha Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa Mwaka 2015/2016.

Waziri wa Fedha:

Hotuba ya Kuwasilisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2015/2016.

III. **MASWALI:**

Ofisi ya Rais, Tawala Za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:

17. MHESHIMIWA SALEH NASSOR JUMA (Jimbo la Wawi) -
Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,
Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:

Kwa kuwa kambi ya chuo cha mafunzo yenye wanafunzi tisa kwa sasa, iliyoko Kengeja ni miongoni mwa vyuo vya mafunzo vya SMZ. Na kwa kuwa majengo yote yaliyoko katika chuo hicho ni mabovu, yaliyokosa kiwango na yasiyostahiki kuwekwa mahabusu wala Askari kutokana na uchakavu mkubwa uliopo katika majengo hayo.

Je, ni lini Serikali itamalizia kujenga lile jengo moja lililoanza kujengwa kwa juhudi za askari wetu pamoja na kujenga angalau jengo moja la Utawala.

Wizara ya Mifugo na Uvuvi:

45. MHESHIMIWA JAKU HASHIM AYOUB (Jimbo la Muyuni) -
Atamwuliza Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi:

Kwa muda mrefu joshu la mifugo la kisakasaka limekuwa halifanyi kazi kutokana na kukosekana kwa “pump” na kusababisha mifugo kuchinjwa bila ya kusafishwa na dawa, jambo ambalo linaweza kusababisha maradhi ya mifugo na kuathiri wafugaji wetu Zanzibar.

- (a) Kwa nini Serikali imeshindwa kuondoa tatizo hilo karibu nusu mwaka sasa na kusababisha mifugo kuendelea kuchinjwa bila ya kudhibitiwa maradhi ya mifugo.
- (b) Ni lini Serikali itarudisha huduma hiyo badala ya joshu hilo kuendelea kubaki kama pambo kinyume na azma ya kujengwa kwake.
- (c) Mifugo inayoingia Kisakasaka inakaguliwa vipi kabla ya kuchinjwa ili kudhibiti maradhi ya kuambukiza.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Ikulu na Utawala Bora:

Kwamba Baraza hili lifikirie na kuukubali Mpango wa Maendeleo wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa Mwaka 2015/2016.

Waziri wa Fedha:

Kwamba Baraza hili lifikirie na kuyakubali Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Kazi za Kawaida na Maendeleo ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa Mwaka 2015/2016.

Zanzibar,
13 Mei, 2015.

(Yahya Khamis Hamad)
KATIBU WA BARAZA.